**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Nane – Tarehe 17 Septemba, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis:**

Hoja ya Mjumbe kuhusu kuliomba Baraza la Wawakilishi kupitisha Azimio maalum la kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kauli yake ya mgombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwaka 2025 kuwa mwanamke.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

66. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

    Kuna masoko mengi ambayo yamekuwa yakitoa huduma kwa wananchi kwa muda mrefu mfano Mikunguni, Kwahajitumbo lakini kwa sasa hayako katika hali nzuri.

    (a) Je, Serikali inachukuwa hatua gani ya kuyaimarisha masoko hayo.

(b) Je, maeneo ya masoko bado yapo salama na hayajaathiriwa.

(c) Je, ni lini Serikali itayaimarisha masoko hayo kwa kujenga majengo ya kisasa.

**<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>**

46. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Katika vikao vya Bajeti vilivyopita (2021/2022) vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge lilipitisha kodi ya miamala inayohusiana na utumiaji na upokeaji wa fedha kwa mitandao ya simu na kodi hiyo imeanza kutumika tarehe 15/07/2021.

(a) Je, Serikali yetu ya Zanzibar nayo imeridhia jambo hili.

(b) Je, Serikali haioni kuwa kufanya hivyo ni kuzidi kuwaongezea wananchi wetu mzigo mgumu wa maisha.

**<u>Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:</u>**

138. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Serikali imekuwa ikilipa kipaumbele zao la mwani kwa kuwa linachukua nafasi kubwa katika shughuli za wananchi wa ukanda wa pwani hasa wanawake. Hata hivyo, wazalishaji wa mwani wapya mara nyingi wanashindwa kupata nyenzo muhimu za uzalishaji kama vile kamba, maboya, vitaitai, mabero na vitendea kazi vyengine vya uzalishaji mwani.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kurahisisha upatikanaji wa vifaa hivyo kwa wajasiriamali wadogo wa mwani.

(b) Serikali inawasaidiaje wakulima wapya wa mwani ambao hawana mtaji wa kuanzia kilimo cha mwani.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

69. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Hivi sasa Zanzibar tumeshuhudia maendeleo ya vyombo vya habari binafsi vinatoa mchango mkubwa katika kuwapatia taarifa wananchi.

(a) Je, kwa sasa jumla ya vyombo vya habari vingapi vimesajiliwa Zanzibar.

(b) Je, Serikali inasaidiaje kutatua changamoto zinazovikabili vyombo hivyo.

(c) Je, ni lini Serikali itafikiria kupunguza gharama za usajili ili kuwasaidia wenye nia ya kuanzisha vyombo binafsi vya habari.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

26. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Zao la parachichi ni zao linalotegemewa sana katika mikoa mingi ya Tanzania Bara kama zao kuu la biashara na limekuwa maarufu na kuanza kujipatia soko la ndani na nje ya nchi. Zao hili hustawi sana katika maeneo mbali mbali ya kisiwa cha Unguja.

Je, ni lini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar italifanyia utafiti wa kina zao hili na hatimae kuwasaidia wakulima kwa ajili ya kuanzisha kilimo cha parachichi ikiwa ni njia nyengine itakayowasaidia kupunguza umasikini na kujiongezea kipato.

123. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Pamoja na jitihada za Serikali katika kuendeleza kilimo cha mpira na uvunaji wake, kumekuwa na uharibifu mkubwa wa mazingira unaotokana na kiwanda cha mpira katika maeneo ya Mwane, shehia ya Maziwani ambacho kinatumia nishati ya kuni za mwembe.

(a) Je, Serikali imewahi kutathimini kiasi cha athari ambayo wakaazi wa maeneo hayo wanaipata kutokana na uharibifu huo wa mazingira.

(b) Je, ni lini Serikali itaboresha mazingira ya kiwanda hicho kwa kukipatia huduma stahiki za umeme na kuondokana na matumizi ya kuni.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

47. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Hivi karibuni Waziri anayehusiana na mambo ya nishati Tanzania Bara alitangaza mubashara akiwa Bungeni kuwa malipo ya gharama za kuunga umeme ni Tsh. 27,000/- tu na hakuna gharama ya malipo ya nguzo. Kwa kuwa Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Je, Serikali haioni iko haja ya kuangalia upya malipo ya gharama za uungaji pamoja na malipo ya gharama ya ununuzi wa nguzo ili angalau tuende sambamba na wenzetu wa Tanzania Bara.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

49. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Yako maeneo ambayo Serikali huchukua mali ghafi ya mawe na kokoto kama vile Muwambe, Micheweni, Vitongoji na Kibele. Kwa kuwa maeneo haya ni muhimu sana na barabara zake ni mbaya.

Je, ni lini Serikali itayaonea huruma maeneo hayo kwa kuyatengenezea barabara zake hizo.

141. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika ujenzi wa barabara inayounganisha Mzambarauni na Finya, tathimini kwa ajili ya malipo ya fidia ya watu waliovunjiwa nyumba zao na kuharibiwa mazao na vipando vyao ilifanyika, na kupitia Afisa Mdhamini mwenye dhamana ya mawasiliano Pemba, wananchi waliahidiwa kulipwa. Hata hivyo, hadi leo

wahusika hawajalipwa wala kupewa maelezo na sababu ya kucheleweshwa kulipwa.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kilikusudiwa kulipwa wananchi kwa ujumla kama fidia ya kuvunjiwa nyumba zao na kuharibiwa mazao na vipando vyao.

(b) Je, ni kwa nini kumekuwa na ucheleweshwaji wa malipo hayo kwenda kwa wananchi.

(c) Je, ni lini fidia hiyo na faida yake ya kucheleweshwa vitalipwa kwa wananchi na kwa utaratibu gani.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

55. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Moja ya lengo kuu la Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 ni kuwapatia wananchi ardhi na makazi bora. Hivyo, mara tu baada ya kufanikiwa kwa Mapinduzi hayo, Rais wa kwanza na muasisi wa Mapinduzi hayo marehemu Abeid Amani Karume aliwagawia wananchi eka tatu (3) ili waweze kufaidi matunda ya Mapinduzi hayo na kuwaondoa katika umasikini uliokithiri.

(a) Kwa kuwa muda mrefu umepita tangu kuchukuliwa kwa hatua hiyo, Je Serikali imeweza kufanya tathmini ya mafanikio ya lengo hilo.

(b) Ni ekari ngapi zimetolewa tangu uamuzi huo ulipofanyika na ngapi zimeshauzwa na kutumika kwa matumizi mengine.

(c) katika Wilaya ya Magharibi “A” wananchi waliokuwa wakiishi katika eka za watu wamefukuzwa ingawa wengi wameishi zaidi ya miaka thalathini katika maeneo hayo. Je, Serikali ina kauli gani juu ya kadhia hii.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

86. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kwa kuwa mapato ya Zanzibar yanategemea sana Sekta ya Utalii, na kwa kuwa uingiaji wa watalii nchini unategemea pamoja na mambo mengine, vivutio vya watalii vilivyomo nchini.

(a) Je, Zanzibar iko nafasi ya ngapi ukilinganisha na nchi nyengine za Afrika kwa idadi ya vivutio vya watalii.

(b) Je, ni vivutio gani vinavyowavutia zaidi watalii kuja Zanzibar.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuviimarisha zaidi vivutio hivyo ili kuongeza idadi ya watalii na mapato ya nchi kama ilani ya CCM inavyoelekeza.

**<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>**

76. MHESHIMIWA HABIBU ALI MUHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo na Amali:

Tunaamini kwamba kila mwaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inaandaa ripoti ya tathmini ya matokeo ya mitihani kwa ngazi zote kuanzia daraja la nne (4) hadi daraja la kumi na nne (14) lakini bado skuli za Zanzibar zinachukua nafasi za mwisho, kutokana na hali hiyo basi ni vyema kutuelewesha yafuatayo.

(a) Je, tathmini zipi zinazofanywa kwa angalau miaka mitano.

(b) Je, mikakati gani Wizara yako imeipanga ili kuboresha matokeo ya mitihani kwa wanafunzi wa Zanzibar.

129. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Juhudi za Serikali kuhakikisha kwamba watoto wa skuli za maandalizi hawaendi masafa makubwa kusoma ni za kupongezwa. Hata hivyo, skuli ya maandalizi iliyopo katika kijiji cha Mlindo ya Pandani ambayo imepasishwa na Serikali, inaendeshwa kwenye baraza ya mtu ya kuazima inayovuja na iliyozingirwa kwa uwa wa makuti. Kwa vile sehemu ya sasa haina sehemu ya kuchezea na skuli ya maandalizi ya Pandani ipo mbali kwa watoto wa umri huo:

(a) Je, Serikali ilitumia vigezo gani kuipasisha baraza hiyo kuwa skuli ya maandalizi.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia watoto hao sehemu salama na rafiki kabla ya mwaka wa masomo wa 2022 kuanza.

(c) Kwa kuwa wananchi wameshapata sehemu bora na salama ya kuwajengea watoto wao mabanda ya Skuli ya Maandalizi ya Mlindo, Je, Serikali inawaahidi wananchi wa Mlindo kuwapatia msaada gani kuhusiana na ujenzi wa skuli hiyo.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

15. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na ongezeko kubwa la maradhi ya watoto wanaozaliwa ya vichwa vikubwa na yale ya mgongo wazi, hali ambayo inaleta hofu kubwa kwa wazazi wa watoto hao.

(a) Je, Serikali inatambua kuwepo kwa tatizo hilo.

(b) Ni sababu gani za kitaalamu zinazopelekea kuongezeka kwa maradhi hayo.

48. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Tatizo la ugonjwa wa mifupa (*Sickle Cell Disease*) limekuwa kubwa sana hapa Zanzibar. Na kwa kuwa dawa za maradhi haya zinapatikana katika hospital ya Mnazi Mmoja pekee.

Je, Serikali haioni kuwa iko haja ya kuandaa utaratibu mahsusi wa kuwapatia dawa hizo hospitali za Wilaya ili kuwaondolea usumbufu wagonjwa ambao hutakiwa kufuata dawa hizo katika hospitali ya Mnazi Mmoja tu.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

71. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda.

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuendelea kununua karafuu katika msimu huu wa 2021/22 kwa bei ya daraja la kwanza kilo elfu 14,000/-, daraja la pili 13,000/- na daraja la tatu elfu 12,000/- lakini kumekuwa na tatizo la uuzaji wa karafuu hizo na namna ya upatikanaji wa pesa.

(a) Je, Mheshimiwa Waziri suala hili ni la kweli.

(b) Je, kwa nini utaratibu wa zamani wa mtu kuuza na kupata pesa zake pale pale umeondolewa.

## IV. **HOJA YA MJUMBE:**

**Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis.**

Hoja ya Mjumbe kuhusu kuliomba Baraza la Wawakilishi kupitisha Azimio maalum la kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kauli yake ya mgombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwaka 2025 kuwa mwanamke.

**Zanzibar,** **(Raya Issa Msellem)**
**17 Septemba, 2021.** **KATIBU WA BARAZA.**